



3SquaresVT

*Mpango wa Vermont wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada
(ilikuwa ikiitwa Food Stamps)*

Msingi

3SquaresVT Ni nini?

- 3SquaresVT husaidia watu wa Vermont waimarishe bajeti zao za chakula na kuhakikisha wanapata kula vyema anagalau mara tatu kwa siku.
- Marupurupu yako ya kila mwezi yanakuja kwa kadi ya EBT (hawala ya marupurupu kupitia umeme) inayotumika tu kama kadi ya benki.
- Kama kila mtu nyumbami kwako ana umri wa miaka 65 au zaidi au anapata Mapato ya Ziada ya Jamii SSI (supplemental security income), unaweza kupata marupurupu yako moja kwa moja kila mwezi kupitia akiba yako ya benki.

Nani aweza kupata Marupurupu ya 3SquaresVT?

- Jamii zenye mapato ya kiwango: Viwango vya mapato vimeongezeka kwa hivyo watu wengi zaidi wa Vermont wanastahili.
- 3SquaresVT is open kwa kila anayestahili, ikiwa ni pamoja na watu binafsi, familia, wazee na walemavu.
- Watu wengi wanastahili kupata 3SquaresVT lakini hawajui.
- Sheria maalum zinarahisisha uwezekano wa jamii yenye mzee au mlemavu kustahili kupokea kupata marupurupu.
- Ili ujue kama wastahili kupata marupurupu, tazama www.vermontfoodhelp.com.

Naweza Kupata Kiasi Gani?

- Marupurupu ya kila mwezi yanategemea mapato na ukubwa wa familia. Jinsi mapato yanavyopungua, ndivyo marupurupu yako ya 3SquaresVT yanavyoweza kuongezeka.
- Kiwango cha juu zaidi cha marupurupu ni **\$200** kwa mtu ambae hajaowa/olewa na hana mapato. Ni **\$368** kwa familia ya watu 4 yenye pato la **\$1000** kwa mwezi (baada ya ushuru).
- Mhudumu wako wa 3SquaresVT atatazama mapato yako na gharama zako za kila mwezi ndipo afahamu kiwango chako cha marupurupu.

Nifanye Vipi Maombi?

- Piga simu **1-800-479-6151** au tazama www.vermontfoodhelp.com upate fomu ya kufanyia maombi.
- Ukihitaji usaidizi kujaza fomu yako ya maombi: Tumia simu yako upige **2-1-1** na uombe uelekezwe kwa **Community Action Agency** ya karibu yako.
- Kama ni mzee, piga simu **1-800-642-5119** upate **Vermont Senior Helpline**.



Vermont Campaign to
End Childhood Hunger

*Ujumbe huu umedhaminiwa kwa kiasi na USDA,
Mpena nafasi tena muajiri kwa usawa.*

4/10/09

 **VERMONT**
DEPARTMENT FOR CHILDREN AND FAMILIES
ECONOMIC SERVICES DIVISION